

# Usawiri wa Ujumi katika Fasihi Simulizi: Uchambuzi wa Ngano za Wahehe

Neema Julius Luhwago

Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania

## Uwasilishaji wa Makala

Kupokelewa: 2025-01-22

Kurekebishwa: 2025-06-30

Kukubaliwa: 2025-07-10

Kuchapishwa: 2025-07-12

## Maneno Muhimu

Sanaa

Fasihi

Fasihi Simulizi

Ngano

Ujumi

## Jinsi ya Kurejelea Makala:

Luhwago, N. J. (2025). Usawiri wa Ujumi katika Fasihi Simulizi: Uchambuzi wa Ngano za Wahehe. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, 3(2), 10-18.

Copyright © 2025



## Ikisiri

Lengo la makala hii ni kujadili namna ujumi unavyosawiriwa katika fasihi simulizi, hususani ngano za Wahehe. Kusawiriwa kwa ujumi katika ngano za Wahehe kupitia vipengele vya ujumi kumeweka bayana uwiano wa vipengele hivyo na jamii husika. Aidha, athari zake kwa jamii husika zimebainishwa. Utafiti uliozaa makala hii ulitumia mbinu za kitaamuli. Data zilikusanywa kwa kutumia njia za uchambuzi matini na mahojiano. Ngano teule zilipatikana kwa kutumia sampuli lengwa. Utafiti na mjadala vimefanywa kwa kutumia Nadharia ya Ki-Marx iliyoasisiwa na Karl Marx na Fredrick Engels. Nadharia hii imekuwa faafu katika utafiti wa makala hii kwasababu inatumia mbinu za kipembuzi katika kuchanganua masuala ya kijamii na kiutamaduni. Matokeo yameonesha kwamba ujumi unaweza kusawirika katika ngano za Wahehe kupitia vipengele vyake, ambavyo ni ujumi katika mtu, asili, vitu, na sanaa. Aidha, vipengele hivyo vinaweka wazi idili za jamii husika zinazotokana na masuala mbalimbali yaliyopo kwenye jamii kama vile uongozi, malezi, ndoa, ufugaji, ulinzi, na kilimo.

## Utangulizi

Sanaa ni ufundi wa kuwasilisha mawazo yaliyomo ndani ya mtu kwa kutumia maumbo au vitu mbalimbali kama vile ususi, ufinyanzi, uchoraji, uhunzi, na lugha. Ufundi huo unapowasilishwa kwa kutumia lugha iliyoandikwa au isiyoandikwa huitwa fasihi (Luhwago, 2018). Kwa mujibu wa Wamitila (2002) fasihi ni usemi wa kisanaa unaotumia lugha kwa njia ya kipekee ili kuwasilisha ujumbe unaogusa hisia, fikra, na maisha ya jamii. Fasihi ni moja, lakini ubainishwaji wake, uhifadhi wake, na namna inavyowasilishwa kwa hadhira huleta tofauti. Tofauti hiyo inatupa tanzu kuu mbili za fasihi, ambazo ni fasihi andishi na fasihi simulizi.

Fasihi simulizi ndiyo fasihi kongwe kuliko fasihi andishi. Senkoro (1985) anaeleza kuwa fasihi simulizi, hususani hadithi ni masimulizi ya kale ambayo hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Lakini tunaweza kujiuliza tukiwa kama wanafasihi wa sasa, je fasihi simulizi inapokelewa tu kutoka katika kizazi kimoja hadi kingine? Je! Ni kweli? Mtazamo huu hauna ukweli kamili kwani fasihi simulizi ni utanzu wa sanaa ulio hai na unaokua (Luhwago, 2018). Mtazamo wa kupokelewa kutoka kizazi kimoja na kingine unaweza kuwa na kiasi cha ukweli lakini si chote, kwani uhai uliopo katika fasihi simulizi huifanya kukua na kubadilikabadilika kutokana na mabadiliko ya wakati na mfumo wa maisha ya jamii husika. Makala hii inafasili fasihi simulizi kuwa ni fasihi inayotungwa au kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa hadhira kwa njia ya mdomo au vitendo na huweza kuhusisha vifaa vya kielektroni katika uhifadhi na uwasilishaji wake. Kwa vigezo vya



kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa njia ya mdomo, ngano ni miongoni mwa vipera vinavyojitokeza katika fasihi simulizi.

Wamitila (2004) anaainisha tanzu kuu nne za fasihi simulizi ambazo ni hadithi, semi, ushairi, na sanaa za maonyesho. Katika hadithi, anaainisha vipera vyake kuwa ni ngano, hekaya, hurafa pamoja na masimulizi ya kihistoria na kiasili kama vile visakale, mapisi, tarihi, kumbukumbu, na visasili. Aidha, makala hii imemakinikia utanzu wa hadithi katika kipera cha ngano ambacho kimejitokeza zaidi katika hadithi za Wahehe.

Ngano ni hadithi za kimapokeo ambazo hutumia wahusika kama vile wanyama, wadudu, mimea, au watu kusimulia tukio au kisa fulani chenye mafunzo kuhusu maisha (Sanga, 2021). Ipo mitazamo mbalimbali kuhusu aina hii ya hadithi. Wapo wanaoona kuwa ngano ni kisawe cha hadithi fupi simulizi za kimapokeo (Wamitila, 2004; Senkoro, 2011). Aidha, wapo wanaoona kuwa ngano ni aina mojawapo ya hadithi fupi simulizi (Madumulla, 2009). Makala hii inafafanua ngano kama hadithi fupi za kimapokeo zinazotumia wahusika kama wanyama, mazimwi, wadudu, mimea, na watu kuonya au kuelezea masuala mbalimbali ya maisha katika jamii husika. Miongoni mwa mambo hayo yanayosawiriwa katika ngano ni ujumi.

Ujumi ni dhana pana ambayo imefafanuliwa na wanafalsafa wengi tangu kale. Plato (427-347), mwanafalsafa wa Ugiriki ya kale aliyeishi miaka ya kabla ya kuzaliwa kwa Masihi aliutazama ujumi kama uzuri wa kazi za kisanaa. Aidha, ujumi ni tafsiri ya neno la Kiingereza "*Aesthetics*" ambalo limetokana na neno la Kigiriki "*Aesthetic*" kwa maana ya uzuri wa sanaa unaopambanuliwa katika hisi za akilini (Mihale, 2011). Sanga (2021) anaeleza maana ya ujumi kuwa ni tawi la falsafa linalochambua kanuni na sheria za Sanaa zinazolenga uwelewa wa uzuri, ubaya, ladha na thamani ya Sanaa. Naye Kant (1928) aliweza kulitafsiri neno hilo katika lugha ya Kiingereza kama "*aesthetic*" na sasa linatumika katika maandiko mengi. Hadi kufikia katikati ya karne ya 20 tafiti kuhusu ujumi zimepanuka na kutumika katika nyanja mbalimbali kama vile falsafa, saikolojia, sosholojia, na sanaa (Barret, 2012). Ujumi kama taaluma inayohusika na kutathmini uzuri na ubaya wa sanaa kwa kuzingatia kanuni au sheria mahususi, huweza kujitokeza katika matawi mbalimbali ya sanaa, ikiwamo fasihi.

Kagan (1975) anaona kuwa ujumi umeathiriwa na nyakati za kihistoria kwa sababu kila kipindi cha kihistoria ujumi huchukua sura yake inayoakisi mfumo wa jamii husika. Kwa mfano, ujumi ulipita katika hatua za ujima, utumwa, umwinyi, ubepari, ujamaa, na ukomunisti ambapo hatua hizo zinaonesha mabadiliko ya kiidili na sanaa za jamii fulani au tabaka husika. Sanga (2021) katika kuuelezea ujumi wa kiasia anaeleza kuhusu athari za kikoloni kuwa kuna mataifa ya Kiafrika yanashindwa kuutambua ujumi wao wa asili kutokana na athari za kikoloni. Hoja hii inaweza kukubalika kwani jamii nyingi za Afrika zina utamaduni wa kimahuluti. Aidha, makala hii inatoa mwanga kwa jamii zingine kuweza kutumia ngano kuusawiri ujumi wa za jamii zao.

Sanga (2021) anaifafanua dhana ya ujumi kwa kuuhusianisha na vipengele vya utamaduni, tabia, na maamuzi ya akili katika kuthamanisha ujumi. Anasisitiza kuwa ili kuufahamu ujumi wa jamii husika hatuna budi kuuhusianisha na tamaduni. Dhana ya uzuri wa kiujumi inatakiwa kutumiwa kwa uangalifu sana, kwani kuna uzuri wa aina nyingi. Sanga (2021) anaeleza kuwa kuna uzuri wa mila, desturi, na kaida; na mwingine ni ule unaopatikana katika lugha au maneno. Anaendelea kueleza kuwa ikiwa uzuri utashughulikiwa katika mila, desturi, na kaida basi utahesabiwa kuwa chini ya *ethos* (ethics) na iwapo utashughulikiwa katika lugha au maneno utahesabiwa kuwa chini ya *logos* (word). Kutokana na dhana hii, tunaweza kupata mawanda mawili ya uzuri kwa kuangalia sehemu kuu mbili, yaani "*ethos*" inayoshughulikia uzuri unaotokana na malezi, mazoea, kaida, na



hata utamaduni kama vile kuvaa vizuri, kulima, kuvua, na kufuga. Pia, “logos” inayoshughulikia uzuri unaotokana na maneno, kusema vizuri, na kuimba vizuri. Usawiri wa ujumi katika fasihi simulizi, hususani ngano za Wahehe unachangia kuweka wazi idili za jamii husika katika kipindi hiki cha sayansi na teknolojia. Yafuatayo ni maelezo mafupi kuhusu jamii ya Wahehe.

### **Maelezo Mafupi kuhusu Jamii ya Wahehe**

Kutokana na makala hii kushughulika na suala la ujumi na namna unavyosawiriwa katika ngano za Wahehe, hatuna budi kuifahamu historia fupi ya jamii hii. Wright (1961) anaeleza kuwa Wahehe ni miongoni mwa jamii zinazopatikana nchini Tanzania. Kiasili, wanaishi katika wilaya za Kaskazini mwa mkoa wa Iringa, yaani Iringa, Kilolo, na Mufindi. Aidha, ni moja kati ya jamii zinazodhaniwa kuwa zilitokea kwenye Bonde la Mto Rufiji. Kasebele (2024) anaeleza kwamba Lugha ya Kihehe imegawanyika kiasi fulani katika lahaja (matamshi) mbalimbali. Kwa namna fulani, inafanana kimatamshi na kimaana na lugha ya Kibena iliyopo Mkoani Njombe. Aidha, jamii hii imeendelea kukua na kusambaa katika maeneo mengine yaliyo nje ya mkoa wa Iringa kama vile Wahehe waliopo katika Wilaya ya Mpwapwa, Mkoani Dodoma. Kihistoria, Wahehe ni maarufu kwa jinsi walivyopambana na Wajerumani walioteka maeneo yao katika kipindi cha kuingia kwa wakoloni. Hii inajidhihirisha katika mapigano ya Lugalo (1891) yaliyoongozwa na Jemedari wao Mkwawa. Willoughby na wenzake (2019) wanaeleza kuwa Mkwawa alipata umaarufu katika uongozi wake hasa kwa namna alivyoongoza vita vya Wahehe na Wajerumani.

### **Nadharia ya Utafiti**

Maudhui ya makala hii yanaongozwa na Nadharia ya Ki-Marx. Waasisi wa nadharia hii ni Karl Marx na Fredrick Engels (Mushengyezi, 2003). Nadharia hii ya Ki-Marx ni ile inayotumia mbinu za kipembuzi katika kuchanganua masuala ya kijamii na kiutamaduni (William, 1977). Misingi ya nadharia hii iliyotumika katika uchanganuzi wa data ni mitatu. Mosi, kazi ya fasihi ni matokeo na athari ya mfumo-jamii na matabaka yake. Aidha, huona kuwa fasihi kama zao la jamii hubeba mambo yote yaliyomo katika jamii hiyo na kamwe haiwezi kujitenga na jamii. Pili, masuala ya kiitikadi katika jamii nayo yana umuhimu mkubwa. Mushengyezi (2003) anasema kuwa itikadi hubeba mawazo, taswira, utamaduni, miiko, imani, na kanuni zinazofungamana na shughuli zote za kijamii. Tatu, sanaa, ikiwemo fasihi, huathiri kwa kiwango kikubwa maisha ya jamii. Vilevile, nadharia hii huyatazama maudhui ya fasihi kuwa na dhima ya kuchochea hisia na utashi katika kuleta mabadiliko katika jamii; na kazi ya fasihi huwa ni chombo muhimu katika kuelimisha. Hivyo basi, kupitia misingi ya nadharia hii mtafiti amevichunguza vipengele vya kiujumii vilivyomo katika ngano za Wahehe.

### **Methodolojia**

Makala hii imeegemea katika mbinu za kitamuli. Hii ni kutokana na utafiti huu kuhusisha fikra na ufafanuzi katika dhana mbalimbali (Ponera, 2019). Mahojiano yalifanyika kati ya mtafiti na wazee wa jamii ya Wahehe walioko wilaya ya Kilolo, Mkoani Iringa. Usampulishaji lengwa ulitumika katika kuchagua watafitiwa. Mtafiti aliwachagua wawakilishi kulingana na wanavyokidhi haja ya utafiti. Mtafiti alitumia sampuli lengwa ya wazee 10 waliochaguliwa kwa mpangilio rasmi. Wazee hao walikuwa wale wenye umri kuanzia miaka 60 na kuendelea. Wazee wa umri huo walichaguliwa kutokana na kuamini kwamba wazee walioishi muda mrefu wanafahamu mambo mengi kuhusiana na maisha katika jamii husika. Aidha, idadi hiyo ya Wazee kumi ilituliwa kwasababu wazee hao walikidhi matakwa ya data zilizohitajika katika utafiti huu. Kila mzee alisimulia ngano moja na mtafiti alizirekodi ngano hizo. Mtafiti na alirekodi ngano kumi kupitia vinasa sauti na kuziandika kwa lugha ya Kihehe na kuzitolea tafsiri kwa lugha ya Kiswahili. Mtafiti aliweza kuzitolea tafsiri ngano hizo, kwani naye ni miongoni mwa wanajamii husika na ana umilisi



wa lugha ya Kihehe na Kiswahili. Aidha, ngano tano tu ndizo zilizotafsiriwa na hatimaye kufanyiwa uchambuzi kama matokeo ya utafiti. Kutafsiriwa kwa ngano tano tu kulitokana na kujirudiarudia kwa maudhui ya ngano zilizokuwa zikisimuliwa na wazee husika. Kujirudiarudia huko kulisababishwa na uwepo wao katika eneo moja la makazi. Hili lilifanyika ili kuweza kupata urahisi wa kufafanua vipengele vya kiujumi vinavyojitokeza katika kila ngano na athari zake kwa jamii husika. Data zilizopatikana zilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji wa maudhui katika ngano zilizochaguliwa. Data hizo zilifafanuliwa kwa kufuata mtiririko wa vipengele vya kiujumi vilivyojitokeza katika ngano zilizofanyiwa uchambuzi. Aidha, ufafanuzi huo uliweza kuwakilisha maana mahususi katika lengo kuu la makala hii, ambalo ni kuusawiri ujumi katika ngano husika.

### Ngano za Wahehe na Tafsiri zake kwa Kiswahili

Sehemu hii inawasilisha ngano tano za Wahehe zilizotafitiwa ambazo mtafiti alizitafsiri kwa Kiswahili. Ngano hizo ni *Isungula na Umunyamugunda gwa Mangogo*, *Umunu na Avanakwe Vavili Vakwamisi*, *Chamulige Avagenda Kilo*, na *Umukwamisi na Isenga*.

#### 1. *Isungula na Umunyamugunda gwa mangogo*

*Paidaha kwekwina munu yeealimite umugunda gwa mangogo. Isungula yabitige kuhisa amangogo mbeepali pamihye. Pembekuchee umunyamugunda afikige amakombo ga amayavilo ga mangogo na amabandi ga mangogo agalifilwe. Kimunyi ikimwi umunyamugunda ahele kutega ulutego pagati pa mugunda gwakwe. Umutego ugo gwali mufihe na amangogo amayave. Isungula pe yifikite pamihye ndawe ye yisovye yafikite amanggo amakong'ase. Kwa uwupumu Isungula yadibuche neke yivange ukudakula kono weyikelye pakutigila umunya mugunda asemilwe. Kwa wupifu Isungula yadakwe neke amangogo gakepite ulugelonikise na umutego. Neke Isungula yagwilye mulutego. Umunyamugunda pe afikite awulige Isungula neke ategule kukaye swe yiva nyama.*

#### Tafsiri: Sungura na Mwenye Shamba la Karanga

Hapo zamani za kale, kulikuwa na mtu mmoja aliyekuwa amelima shamba la karanga. Kila siku jioni sungura alikwenda kuiba karanga. Kila kukicha mwenye shamba alipokwenda shambani alikuta mashimo ya karanga zilizochimbwa na maganda ya karanga zilizoliwa. Siku moja, mwenye shamba akatega mtego katikati ya shamba lake, ambapo mtego huo aliufunika na karanga zilizochimbwa. Sungura alipokuja jioni kama ilivyo ada, alikuta rundo la karanga. Kwa hamaki, alizirukia na kuanza kuzila, huku akiwa na furaha kuwa mwenye shamba amezisahau. Alipokuwa akiendelea kula, zile karanga ziliendelea kupungua hadi kufika mtegoni. Ghafla sungura akanaswa mtegoni. Mwenye shamba alipokuja alimwua na kumchukua hadi nyumbani kwake akamfanya kitoweo.

#### 2. *Umunu na Avanakwe Vavili Vakwamisi*

*Pakatali, pe pina umunu yeeinavana vavili vakwamisi. Umunu uyu ikalige pamwi na vanakwe peminyi ye yina wugaya wa ululenga. Avegasi avolofu vakanige avanawo ukubita kunega ululenga viyena kukisela. Ino umunu uyu mbepali pamitwa aibita kumugunda na ukuvatuma avana kunega ululenga kukisela. Ikimunyi ikimwinga avakwamisi iwo vahafile ukubita kukisela kwa kuva vihesigige mung'asi. Vafikite kukisela peye avavina mbevali vanesile ululenga neke vapilukeukwawo. Pe vanegite ululenga kukisela vagiweve imingigi mukisela neke vavange ukwihesigila hambi vibate. Ikimunyi pe kifikite udadao apitwike kukaye neke awone avanakwe sivala piluka neke pe alamule ukuninila kukisela. Afisile mung'asi awusise avanu ve vavasele*

*avanakwe. Pe ahele kukisela afikite avanakwe vatagike vakwengela mululenga. Papene pe iwike ulukani lwe alonzile umunzagila pakutigila avana se valabita viyena kunega ululenga kukisela.*

**Tafsiri:** Mtu na Watoto Wake Wawili wa Kiume

Hapo zamani za kale palikuwa na mtu aliyekuwa na watoto wawili wa kiume. Mtu huyu aliishi pamoja na watoto wake katika kijiji ambacho kilikuwa na shida ya maji. Wazazi wengi waliwakataza watoto wao kwenda kuteka maji kisimani peke yao bila kuwa na mtu mzima, kwani kisima kilikuwa kirefu sana. Lakini mtu huyu kila asubuhi huenda shambani na kuwatuma watoto kwenda kuteka maji kisimani. Siku moja watoto hao walichelewa kufika kisimani, kwani walikuwa wakicheza njiani. Wakafika kisimani wakati ambao watu wazima wote wameshateka maji na kurudi makwao. Walipokuwa wakiteka maji kisimani, waliona vivuli vyao ndani ya kisima, wakaanza kuchezea wakitaka kuvishika. Ilipofika alasiri, baba yao alirudi nyumbani akakuta watoto wake hawajarudi. Ndipo akaamua kuwafuata kisimani. Alipokuwa njiani, aliwauliza watu waliowafahamu watoto wake. Alipofika kisimani aliwakuta watoto wake wanaelea juu ya maji wakiwa wamekufa. Ndipo alipokumbuka kiongozi wa kijiji alivyowaambia kuwa watoto hawaruhusiwi kwenda kisimani peke yao.

### 3. *Che Chamuwulige*

*Kwekina munu ilitawa lyakwe akemelwigwe Chamuwulige. Umunu uyo vevamkanite alemwage ukwingisa umoto kuuvaso nave iwona ng'ala. Ikimunyi ikimwina yatonyite indonya ndzolofu/ngomi. Sweno kwiva na ing'ala nzolofu hilo. Chamulige aasemilwe chevevamlonje avakukwe. Sweno akwingisa umoto kuuvaso neke adinde imilyango na ifimbwilya mbefili. Pakilo mugali kwe kwina ifuguto ng'ali neke alemwe ukwehela kwa ikisemwa chakwe. (Ulusimo ulu lukutwigisa pakutigila tuvelage na lwiwu).*

**Tafsiri:** Kilichomuua

Kulikuwa na mtu aliyeitwa Chamuwulige (kilichomuua). Wazee walikuwa wamemkataza kuwa hata akiona amepatwa na baridi asije akaingiza moto chumbani anakolala. Siku moja mvua kubwa sana ilinyesha, kukawa na baridi kali. Chamuwulige akasahau ushauri wa babu zake. Akaingiza moto chumbani anakolala na akafunga mlango na madirisha yote. Katikati ya usiku joto likawa kali, akashindwa kupumua hadi kufa kutokana na usahaulifu wake. (Hadithi hii inatufundisha kutunza kumbukumbu).

### 4. *Avagenda Kilo*

*Pepina avanu vavili vevina ulugendo lwapatali lwa kugenga ikilo mbekili. Pekifikite ikilo uyumwi amlonje umuyagwe pakutigila vasuke vagonase pono. Umuyagwa palongilwe ulukani ulu abihye. Atige idaha kwekwina avanu vevagonise imitava gijo neke inyumba sivagwile pakilo neke vafwe. Kwe kwina ndonya nzolofu sweno vibitaga na ulugendo lwawo. Kwa kuva kwekwina lwisa hilo valamwe vagone mwihala. Pakilo pe vagonite ilififi lyasile linyugule iliwoko ilya yula yalabihe ukuvasa mukaye. (Ulusimo ulu lukutwigisa tulemwage ukugenda pakilo).*

**Tafsiri:** Watembea Usiku

Palikuwa na watu wawili waliokuwa wakisafiri safari ndefu ya kutembea usiku kucha. Ilipofika jioni mmojawapo akamwambia mwenzake tuombe mahali kwa wenyeji ili tulale. Mwenzake alipoambiwa hivyo, akakataa kutokana na sababu kuwa siku za



nyuma maeneo hayo nyumba ziliwahi kuwadondokea watu usiku huku wamelala wakafa. Hivyo, waliendelea na safari; kwa kuwa kulikuwa na giza waliamua kulala porini. Walipokuwa wamelala, fisi akaja akanyofoa mkono wa yule aliyekuwa amekataa. (Hadithi hii inatufundisha tusipende kutembea usiku).

#### 5. Umukwamisi na Isenga

*Kwe kwina kimunyi kimwinga umwegasi amulonje umuswamuve pakutigila valowoke na isenga umukonga vabite umwambu gwa kavili. Isenga iyo ye yina ngwada ndodo. Isenga yila, yalowokige umukonga na kupiluka. Umuvaha amuwusise umuswamuve pakutigila kumbi ndawuli isenga yipiluka? Umuswamuve amulonje udade pakutigila pewisaka ing'inayo yilowoke longose ingadwa. Pe vagisile ndahiyo; isenga yalowike umukonga. Umuvaha yula amuwulige umuswamuve ukuva amwigise. (Ulusimo ulu lukutwigisa pakutigila tuvapulikage avana navo vana ng'ani nofu).*

**Tafsiri:** Kijana na Ng'ombe

Siku moja mzee mmoja alimwambia mtoto wake wa kiume tuvuke na ng'ombe hadi ng'ambo ya mto. Yule ng'ombe alikuwa ana ndama mdogo. Basi yule ng'ombe alikuwa anavuka mto na kurudi. Mzee akamwuliza kijana wake, kwani vipi? Yule kijana akamwambia, "ukitaka huyu ng'ombe avuke, kwanza tumvushe ndama wake". Walipofanya hivyo, yule ng'ombe alivuka. Yule mzee akamwua kijana wake kwa kuwa alimfundisha. (Hadithi hii inatufundisha kuwasikiliza hata watoto kwani wanaweza kuwa na ushauri mazuri).

#### **Vipengele vya Ujumi Vilivyomo katika Ngano za Wahehe**

Katika ngano zilizochaguliwa na kutafsiriwa, uchambuzi wake umefanywa kwa kuzingatia misingi ya Nadharia ya Ki-Marx. Vipengele vikuu vinne vya ujumi kama vinavyoelezwa na Baumgarten (1750/2020) vimefafanuliwa. Vipengele hivyo ni uzuri katika mtu, uzuri katika asili, uzuri katika vitu, na uzuri katika sanaa. Baumgarten anaeleza kuwa ujumi ni kipengele kinachoweza kutambulika kwa hisia, sura, mwili, na tabia ya kimaadili ya nje na ndani ya mtu (tabia njema).

Katika asili, anaeleza kuwa uzuri wa asili unaweza kufikiwa kupitia hisia zetu na uwezo wetu wa kutambua na kufurahia mandhari ya asili na viumbe hai. Aidha, ujumi katika asili unakamilishwa na maelezo ya kihisia ya watu kuhusu mazingira yao. Katika vitu, ujumi unaweza kutazamwa kulingana na uwezo wa mtu kutambua na kufurahia maumbo yao, rangi, na muundo. Hii ni kwa sababu uzuri katika vitu unategemea hisia za mtazamaji na namna anavyovitafsiri au kuvielewa na kuvitumia. Vilevile, katika sanaa ujumi anauelezea kwamba sanaa ni njia ya kipekee ya kujieleza, na inahitaji ufanisi wa kihisia na ubunifu. Sanaa ni utendaji wa ubunifu ambapo mtunzi au msanii anatomia vifaa na mbinu za sanaa ili kuleta hisia za uzuri katika mazingira yake kwa kutumia mtindo na mbinu maalum za uumbaji.

Vipengele hivi vya ujumi vinajitokeza katika ngano za Wahehe kama ifuatavyo: Ngano namba 1, kwenye asili tunapata mandhari au mazingira ya ardhi iliyopo na viumbe hai viishivyo ndani yake. Kutokana na kuwapo kwa ardhi, uzuri wake wa asili kwa binadamu na wanyama ni pale wanapoitumia kupata mahitaji yao. Binadamu anaitumia ardhi kwa kulima na kupata mazao ya chakula na biashara. Wanyama nao wanapata chakula kutokana na mazao yanayolimwa na binadamu. Aidha, ubaya katika asili unajitokeza kutokana na mwingiliano wa umiliki, hasa pale ambapo Sungura anakwenda kwenye shamba la binadamu na kula mazao yake. Jambo hili linamfanya binadamu kutega mtego na kumkamata Sungura na kumla. Hivyo, binadamu anaendelea kuifurahia asili, kwani anavitawala viumbe kama wanyama. Katika ngazi ya mtu, uzuri



unajitokeza pale ambapo mtu huyo anajitahidi kulinda mali zake ili zisiharibiwe na wanyama. Katika vitu, uzuri unajitokeza pale mtego unapotumika kama silaha ya kumkamata Sungura aliyekuwa anaharibu mazao ya binadamu. Katika sanaa ya vitu, uzuri unajitokeza kwa ubunifu wa binadamu kutengeneza mtego.

Katika ngano namba 2, kuna maudhui yanayoendana na msingi wa Nadharia ya Ki-Marx unaoelezea athari ya sanaa katika mfumo wa jamii husika. Hili linajidhihirisha katika asili, uzuri unaonekana kwa binadamu kama kiumbe asili kuyatumia mazingira yake kukidhi mahitaji muhimu ili kuishi. Aidha, mazingira yanapokuwa na upungufu wa baadhi ya vitu muhimu humlazimu binadamu huyo kuyaimarisha kwa kuyawekea au kutafuta vitu vinavyokosekana. Kwa mfano, katika jamii ya Wahehe kuna maeneo ambayo yana uhaba wa maji; hivyo, jamii hiyo hulazimika kuchimba visima ili kupata maji kwa matumizi yao ya kila siku. Katika mtu, uzuri tunaupata kwa jinsi anavyojishughulisha ili kupata chakula. Aidha, jamii ya Wahehe imejengwa kwenye idili za ushirikiano katika shughuli mbalimbali, ikiwamo kilimo na kuwalinda watoto bila kujali ni watoto wa nani. Pia, jamii hii inaheshimu viongozi; inapotokea kwamba mtu amekiuka maelekezo ya kiongozi, basi akipatwa na matatizo huchukuliwa kwamba ni yeye mwenyewe ameyataka matatizo hayo. Mfano mzuri ni baba alipokiuka kwa kuwaruhusu watoto wake kwenda kuteka maji kisimani peke yao ilhali ni wadogo, hatimaye wakatumbukia kisimani na kufa. Katika dunia ya vitu, uzuri tunaona kwa kisima kuwa na manufaa ya kumpatia binadamu maji; na ubaya ni pale ambapo kisima hicho kimetumika kuwaua watoto wa binadamu. Katika sanaa, uzuri unapatikana katika ubunifu wa binadamu kuchimba kisima ili kupata maji na kutatua tatizo lililokuwa limemkabili katika mazingira yake. Ubaya ni pale ambapo binadamu anashindwa kulinda kisima kisilete maafa kwake mwenyewe.

Vilevile, katika ngano namba 3 maudhui yake yanathibitisha ukweli wa msingi wa pili wa nadharia kwamba masuala ya kiitikadi katika jamii nayo yana umuhimu mkubwa. Hii inatuonesha namna binadamu anavyoweza kuathiriwa na mazingira yake na kutengeneza mfumo unaoiongoza jamii hiyo. Katika asili, tunaona binadamu akikabiliana na mazingira yake, hususani katika suala la hali ya hewa. Jamii hii ya Wahehe inaishi mazingira ambayo ni ya mvua na baridi. Kiidili, jamii hii inarithisha maarifa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mfano ni pale ambapo Chamuwulige aliambiwa hata akisikia baridi asilale na moto ndani ya chumba anacholala kwa sababu ni hatari. Hata hivyo, alikiukamaelekezo kwa kulala na moto, joto likazidi ndani ya chumba chake akakosa pumzi na akafariki. Katika mtu, uzuri tunaona pia kwenye mahusiano ya wanajamii, wazee na vijana, kupokea maelekezo ya namna ya kukabiliana na mazingira yao na kuweza kukaa salama. Jamii hii imekuwa ikishikilia mfumo huo wa maisha kwa vipindi vyote vya masika na baridi.

Ngano namba 4, inathibitisha msingi wa kwanza wa nadharia hii unaoeleza kuwa kazi ya fasihi ni matokeo na athari ya mfumo-jamii na matabaka yake. Aidha, huona kuwa fasihi kama zao la jamii hubeba mambo yote yaliyomo katika jamii hiyo na kamwe haiwezi kujitenga na jamii. Hili linajidhihirisha katika ngano hii ambapo uzuri wa asili unaonekana kwa mazingira ya hali ya hewa iliyofaafu kwa binadamu na wanyama kama vile fisi. Katika mtu, uzuri unajitokeza kwa binadamu kuishi kwa ushirika na wenzake. Ubaya katika mtu umeonekana pale ambapo mtu mmoja hakumsikiliza mwenzake alipomwambia wasitembee usiku, na alipokiuka na kulala porini akaliwa mkono na fisi. Athari hii inasababishwa na historia ya majanga ya nyuma ambayo yamewahi kuikumba jamii hiyo na kusababisha vifo kwa watu kuangukiwa na nyumba. Tukio hilo limeacha alama kwa mmoja wa watu waliokuwa wanasafiri. Alipolikumbuka lilimsababisha akatae kulala kwenye nyumba za watu wa eneo hilo na kuamua kulala porini. Katika Sanaa ya vitu, uzuri unajitokeza kwa binadamu kuyatumia mazingira yake kiubunifu kwa kujenga nyumba na kukaa



ndani yake. Ubaya ni pale ambapo nyumba zilizojengwa na baadhi ya watu zilikosa ubora zikaanguka na kusababisha vifo kwa watu. Katika hadithi hii, historia ya matukio ya majanga yaliyoikumba jamii siku za nyuma, yameacha athari hasi kwenye mitazamo ya baadhi ya wanajamii.

Katika ngano namba 5, uzuri wa asili unajitokeza pale ambapo binadamu anaishi na wanyama kama vile ng'ombe, ambapo anajipatia maziwa na nyama. Katika mtu unajitokeza kwa uhusiano uliopo kati ya wazee na vijana kuweza kupokea maelekezo ya namna ya kuishi bila kupatwa na majanga. Aidha, ubaya unajitokeza pale ambapo wazee wanaamini kuwa wao ndio wenye uwezo wa kuwashauri vizuri vijana na kuwa watoto hawawezi kuwa na ushauri mzuri kwao. Mfano katika ngano namba 5 ni pale Mzee alipoona aibu baada ya kushauriwa kumvusha ndama kwanza kisha ng'ombe avuke; na alipofanya hivyo walifanikiwa. Ubaya unajitokeza pale ambapo mzee anaamua kumuua kijana wake kwa sababu ya ushauri aliopewa na kijana na ukaleta matokeo mazuri. Kitendo cha mzee kumuua kijana kinaonesha athari hasi ya kimtazamo aliyokuwa nayo.

Hivyo basi, mjadala wa vipengele vya ujumi katika ngano za jamii ya Wahehe umesaidia kufahamu idili za jamii husika. Pia, umeonesha namna binadamu anavyoweza kukabiliana na asili na kuitengeneza ili imfae kwa mahitaji yake ya kuishi.

### **Uwiano Uliopo kati ya Vipengele vya Kiujumi na Jamii Husika**

Willoughby na wenzake (2019) wanaielezea jamii ya Wahehe kwamba imekuwa na ushujaa wa kivita na uongozi mzuri kwa muda mrefu kutokana na mazingira yao kuwa na mapori makubwa na mbuga za wanyama. Aidha, uwezo wao wa ubunifu katika utengenezaji wa silaha kwa ajili ya ulinzi dhidi ya wanyama wakali na maadui zao umekuwa msaada wa ulinzi kwa jamii hiyo. Jambo hili lilidhihirika hata kipindi walipovamiwa na wageni (Wajerumani) katika mipaka yao, ambapo waliweza kupambana nao ili kulinda miji yao.

Maelezo hayo kuhusu asili ya jamii hiyo na uongozi uliokuwepo yanadhihirisha kuwa ujasiri na ulinzi wenye nguvu ni vitu endelevu katika jamii hiyo. Pia, yanaonesha kuwa jamii ya Wahehe huyapa kipaumbele masuala kama vile malezi, kwani mtoto huonekana kuwa mali ya jamii nzima na si mali ya mtu mmoja. Hivyo, hata pale mtoto anapoonekana kwenda kinyume na idili za jamii husika huweza kuadhibiwa na mtu yeyote, hata kama si mzazi wake (Kasebele, 2024). Vilevile, kiburi, kukosa utii kwa wakubwa, na uvivu ni miongoni mwa mambo yanayopigwa vita na wanajamii. Aidha, wanajamii huwalea watoto wao kwa kufuata mila na desturi zao, lugha yao, na kazi zao kama vile kilimo, uwindaji, na uhunzi. Mambo hayo hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Jamii hii hujihusisha na kilimo cha mazao ya chakula na biashara kama vile mahindi, maharage, viazi, njegere, nyanya, na matunda mbalimbali. Hii ni kutokana na mazingira yao kuwa na mvua nyingi na udongo wenye rutuba.

### **Athari za Kiujumi kwa Jamii Husika**

Ujumi unaosawiriwa katika ngano za Wahehe una athari zifuatazo: Mosi, ni utambuzi wa hisia za watu na miitiko yao wanapokabiliana na matukio kadha wa kadha katika maisha kama vile vifo, majanga ya moto, mafuriko, na mengineyo. Jamii hii imekuwa ikitafuta namna ya kuweza kukabiliana na matukio hayo pindi yanapotokea. Aidha, imekuwa na mikakati ya kimafunzo kwa watoto na vijana wanaokua ili kuweza kukabiliana na mazingira husika. Pili, ni umakini katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, hususani kipindi cha baridi na mvua nyingi. Katika msimu wa mvua, jamii hii hutoa mafunzo na msisitizo wa kukumbushana namna ya kujihami na mito au madimbwi ambayo hujaa maji. Tatu, ni mfumo wa mahusiano katika jamii kwa kushirikiana katika masuala ya malezi ya watoto na ulinzi dhidi ya wanyama wakali na waharibifu wa mazao. Kwa



mfano, kutengeneza mitego ili kuwakamata wanyama waharibifu wa mazao, kuchimba visima ili kuondokana na adha ya uhaba wa maji; na hata kuweka sheria na taratibu za matumizi ya visima hivyo. Katika jamii hii, tunaona masuala haya ni jukumu la jamii nzima. Hivyo basi, usawiri wa vipengele vya ujumi katika ngano za Wahehe umesaidia kuitambua jamii hii kwa undani zaidi, hususani katika kutambua idili za jamii husika.

### **Hitimisho**

Upo ukweli wa mambo uliofichika katika maisha yetu ya kila siku. Kupitia uchambuzi wa kiuajumi wa ngano za jamii husika, tunapata ujuzi wa ukweli huo, hususani idili za jamii husika. Jambo hili limedhihirika katika makala hii kwa namna ujumi ulivyosawiriwa katika fasihi simulizi ya ngano za Wahehe. Vipengele vya ujumi vilivyojitokeza katika ngano teule vimeweka wazi mfumo wa maisha wa jamii husika. Kupitia makala hii, imedhihirika wazi namna taaluma ya ujumi inavyoweza kuyaangazia masuala ya mila na desturi za jamii. Hivyo basi, usawiri wa ujumi katika ngano za Wahehe kupitia vipengele vyake umepanua mawanda ya kihakiki katika fasihi simulizi na kwenye taaluma ya ujumi kwa jumla. Vilevile, umeonesha fursa kwa wanataaluma kuendelea kutumia taaluma ya ujumi katika tafiti zao, hususani katika tanzu nyingine za fasihi simulizi kama vile ngojera, nyimbo, majigambo, na ngomezi.

### **Marejeleo**

- Baumgarten, A. G. (2020). *Reflections on Poetry* (First published 1750). Cambridge University Press.
- Kagan, M. (1975). *Aesthetik*. Akademie Verlag.
- Kant, I. (1928). *Critique of Judgement*, Trans. James Creed Meredith. Clarendon Press.
- Kasebele, A. (2024). Ujitokezaji wa Ruwaza ya Shujaa wa Kiafrika katika Kisakale cha Mukwavinyika wa Jamii ya Wahehe. *Mulika* 43(1), 98-116.
- Luhwago, N. (2018). *Nadharia za Fasihi Simulizi*. Fanani Mpole Printer.
- Madumulla, J.S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili Nadharia, Historia, na Misingi ya Uchambuzi*. Mture Educational Publishers Ltd.
- Mihale, K. P. (2011). *Ujumi katika Ushairi wa Mnyampala*. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Mushengyezi, A. (2003). *20<sup>th</sup> Century Literary Theory*. Mukono Bookshop Printing and Publishing Company Ltd.
- Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu*. Central Tanganyika Press.
- Sanga, A. N. (2021). Thamani ya Ujumi wa Kiafrika katika Hadithi Fupi Simulizi za Kiswahili. *Mulika*, 2021, 108-125.
- Senkoro, F. E. M. K. (1985). Fasihi Simulizi na Mabadiliko. *Mulika*, 17, 20-24.
- Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi, Mfululizo wa Lugha na Fasihi*. KAUTTU.
- Wamitila, K. W. (2002). *Mchango wa Fasihi Simulizi katika Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Wamitila, K. W. (2004). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*. Phonex Publishers Ltd.
- William, R. (1977). *Marxism and Literature*. Oxford University Press.
- Willoughby, P., Blittner, K., Bushozi, P., & Miller, J. (2019). "A German Rifle Casing and Chief Mkwawa of the Wahehe: The Colonial and Postcolonial Significance of Mulambalasi Rockshelter, Iringa Region, Tanzania". *African Archaeology*, Juz. Na. 17(2), 23-35.
- Wright, M. I. (1961). *The Hehe*. Institute of Current World Affairs.